

Jifunze Kutotazamia Ukamilifu

Kutazamia ukamilifu hufanya tuhisi kwamba hakuna mtu anayepaswa kukosea, na matokeo ni kwa-mba tutavunjika moyo na kuwavunja moyo wengine. Je, una mwelekeo wa kutazamia ukamilifu? Ikiwa ndivyo, jaribu mambo yafuatayo.

1 TAMBUA TATIZO

Teua eneo ambalo unaonyesha zaidi dalili za kutazamia ukamilifu.



SHULENI

(Unavunjika moyo sana na kukata tamaa kwa sababu hujapata alama za juu kabisa.)



NYUMBANI

(Unapopanga chumba chako unataka kila kitu kiwe mahali pake. Kitu kimoja tu kinapopanguliwa unakasirika.)



URAFIKI

(Huwezi kuvumilia hata kidogo makosa ya wengine—hasa wale unaowaona kuwa marafiki wa karibu.)



MENGINE

Sasa fikiria kuhusu eneo hilo uliloteua.
Ni katika njia gani unaonyesha mwelekeo wa kutazamia ukamilifu?

2 REKEBISHA MTAZAMO WAKO

Biblia inasema kwamba 'hekima inayotoka juu ni yenye usawaziko.' (Yakobo 3:17) Kuhusu eneo ulilotaja kwenye ukurasa wa 1 unaweza-je kuwa na usawaziko zaidi kuhusu yale unayotazamia kufanya au (unayotazamia wengine wafanye)?

► Badala ya

► Ninaweza



3 CHAGUA ANDIKO

Ni andiko gani ambalo linahusu hali yako?

'Uwe na kiasi katika kutembea na Mungu wako.'
—Mika 6:8.

"Kama ungekuwa unaangalia makosa, Ee Yah, Ee Yehova, ni nani angesimama?"—Zaburi 130:3.

"Hakuna mwanadamu aliye mwadilifu duniani ambaye huendelea kufanya mema."
—Mhubiri 7:20.

"Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu."—Waroma 3:23.

"Usawaziko wenu na ujulikane kwa watu wote."
—Wafilipi 4:5.

Andiko ulilochagua linaweza kukusaidiaje kukabiliana na mwelekeo wa kutazamia ukamilifu?

4

CHAGUA MTU WA KUIGA

Unaweza kuchagua nani awe mfano wa kuiga kuhusu usawaziko, na kwa nini?



“Ninapohisi kwamba nimeanza kutazamia ukamilifu, ninajaribu kuwafikiria watu ni-naowaheshimu. Jambo moja ninalo-tha-mini kutoka kwao ni kwamba wananifa-nya nitulie ninapokuwa nao. Ndivyo ninavyotaka wengine wahisi wanapoku-wa pamoja nami na hilo linanifanya niazi-mie kuondoa mwelekeo wowote wa kuta-zamia ukamilifu.”—Anna.



5

JIWEKEE MALENGO

Unaweza kujiwekea lengo gani ili ufaulu kukabili na mwelekeo wa kutazamia ukamilifu?

“Unaposhindwa kufanya jambo kama ulivyopanga, jiambie kwamba ulifanya yote uwezayo. Kazia fikira mambo mazuri. Lione kila kosa kama nafasi ya kujifunza.”—Kara.